TANGAZO LA SERIKALI Na. 497 la Tarehe 21/7/2023

SHERIA YA USAFIRI MAJINI,
(SURA YA 165)

______

# KANUNI

______

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 427)*

______

## KANUNI ZA UKASIMISHAJI WA MAJUKUMU YA USAJILI WA MELI ZA KIMATAIFA KWA TAASISI ZINAZOTAMBULIKA ZA MWAKA 2023

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
MASHARTI YA UIDHINISHAJI WA TAASISI ZINAZOTAMBULIKA

4. Masharti ya uidhinishaji.
5. Mfumo wa usimamizi wa ubora.
6. Ubunifu na uendelezaji.

SEHEMU YA TATU
MAMLAKA YA KUTOA MAELEKEZO KWA TAASISI INAYOTAMBULIKA

7. Uteuzi na usimamizi wa taasisi inayotambulika.
8. Majukumu ya taasisi zinazotambulika.
9. Uidhinishaji wa taasisi zinazotambulika.
10. Makubaliano na taasisi zinazotambulika.

11. Ufuatiliaji wa taasisi zinazotambulika.
12. Wajibu wa Shirika katika kufanya ukaguzi wa meli za nje.
13. Wajibu wa mmiliki wa meli.
14. Wajibu wa Msajili.
15. Kukataa, kufutwa au kusimamishwa kwa uidhinishaji wa taasisi inayotambulika.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA JUMLA

16. Adhabu ya jumla.
17. Kipindi cha mpito.
18. Mipaka ya majukumu ya taasisi inayotambulika.
19. Ushirikiano kati ya taasisi zinazotambulika.
20. Tathmini na utoaji wa taarifa.
21. Ushughulikiaji wa malalamiko.

---

MAJEDWALI

---

SHERIA YA USAFIRI MAJINI,

(SURA YA 165)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 427)*

KANUNI ZA UKASIMISHAJI WA MAJUKUMU YA USAJILI WA MELI ZA KIMATAIFA KWA TAASISI ZINAZOTAMBULIKA ZA MWAKA 2023

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Ukasimishaji wa Majukumu ya Usajili wa Meli za Kimataifa kwa Taasisi Zinazotambulika za Mwaka 2023.

Matumizi

2.-(1) Kanuni hizi zimetengenezwa kwa kuzingatia utekelezaji wa Kanuni ya 1 ya Sura ya XI-1 ya Mkataba wa SOLAS na zitatumika kwa kila meli ya Tanzania na meli nyingine yoyote inapokuwa katika bandari ya Tanzania.

(2) Kanuni hizi zitatumika kwa Taasisi inayotambulika iliyoidhinishwa chini ya Kanuni hizi kutoa, kwa niaba ya Shirika, vyeti kisheria na huduma chini ya sheria husika na mikataba ya kimataifa inayohusu-

(a) usalama wa maisha baharini;
(b) kuzuia uchafuzi kutoka kwenye meli;
(c) viwango vya mafunzo, utoaji vyeti na ufanyaji kazi melini kwa mabaharia;
(d) ukomo wa ujazo;
(e) upimaji wa uzito wa meli;
(f) kanuni za kuzuia meli kugongana baharini; na
(g) haki ya mabaharia kupata ajira nzuri.

(3) Bila kuathiri masharti ya jumla ya kanuni ndogo ya (1), Kanuni hizi hazitatumika kwa-

(a) meli za starehe;
(b) meli za uvuvi;
(c) meli ya ujenzi wa jadi kama vile mtubwi na

mashua; na

(d) meli ya kivita au msaada wa kijeshi.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokua kama muktadha utahiji vinginevyo-

"Azimio la IMO" maana yake ni Azimio lililotolewa na Mkutano Mkuu, Baraza na kila Kamati ya IMO;

"cheti" maana yake ni nyaraka inayotolewa na kampuni iliyokasimiwa kwa niaba ya Shirika kwa mujibu wa Mikataba ya Kimataifa;

"cheti cha daraja" maana yake ni nyaraka inayotolewa na kampuni iliyokasimiwa kuthibitisha uwezo wa meli kwa matumizi na huduma husika kulingana na kanuni zilizopo na zilizowekwa wazi kwa umma na kampuni iliyokasimiwa;

"eneo" maana yake ni mahali ambapo-

(a) ukaguzi unafanyika na kusimamiwa;

(b) idhini za mpango zinatolewa; au

(c) michakato inasimamiwa;

"idhini" maana yake ni kukasimisha madaraka kwa kampuni ili kutekeleza uthibitisho wa kisheria na huduma chini ya sheria husika kwa niaba ya shirika kama ilivyoainishwa kwenye mkataba au katika makubaliano ya kisheria kwa kuzingatia "vipengele vinavyopaswa kuwemo katika mkataba" kama ilivyoelezwa katika Kiambatisho Na. 3 cha Kanuni za Makampuni Yaliyokasimiwa;

"IMO" maana yake ni Shirika la Bahari la Duniani;

"Kanuni za Taasisi Inayotambulika" maana yake ni Kanuni kwa ajili ya taasisi iyotambuliwa kwa mjibu na Azimio la IMO MSC.349(92) lililopitishwa tarehe 21 Juni, 2013 na marekebisho yaliyofuata;

"mamlaka yenye uwezo" maana yake ni wizara, idara ya Serikali au mamlaka nyingine yenye mamlaka ya kutoa na kusimamia utekelezaji wa kanuni, amri au maelekezo mengine yenye nguvu ya sheria kuhusu suala linalohusiana na kanuni husika;

"meli" maana yake ni chombo kinachoelea ambacho kinajiendesha na chenye uwezo wa kubeba abiria au mizigo na inajumuisha maelezo yote ya chombo kinachotumika katika safari kwenye maji;

"meli ya abiria" maana yake ni meli iliyojengwa kwa ajili ya, au ambayo kwa kawaida au wakati fulani inatumika kwa ajili ya kubeba zaidi ya abiria kumi na mbili na inajumuisha meli iliyotolewa kwa ajili ya kusafirisha au kuburudisha wageni katika taasisi yoyote, hoteli, nyumba binafsi wanapolala wageni wa kulipia, nyumba ya wageni au taasisi nyingine yoyote;

"meli ya mizigo" maana yake ni meli isiyokuwa ya abiria;

"meli ya Tanzania" maana yake ni meli iliyosajiliwa au kupewa leseni chini ya masharti ya Sheria kwenye bandari iliyoko katika Jamhuri ya Muungano;

"mikataba ya kimataifa" maana yake ni-

(a) Mkataba wa Kimataifa wa Usalama wa Maisha Baharini wa Mwaka 1974, isipokuwa Sura ya XI-2 ya Kiambatisho chake;
(b) Mkataba wa Kimataifa wa Ukomo wa Ujazo wa Mwaka 1966;
(c) Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Uchafuzi kutoka Melini wa Mwaka 1973/78;
(d) Mkataba wa Kimataifa wa Upimaji wa Uzito wa Meli wa Mwaka 1969;
(e) Mkataba wa Kimataifa wa Kanuni za Kuzuia Kugongana kwa Meli Baharini wa Mwaka 1972; na
(f) Mkataba wa Kimataifa wa Kazi za Baharini wa Mwaka 2006,

pamoja na itifaki na marekebisho yake, na kanuni za lazima zinazohusiana na taarifa za Nchi Wanachama zote wa IMO, katika toleo lake la karibuni lililoridhiwa na Jamhuri ya Muungano;

"miongozo na kanuni" maana yake ni mahitaji ya taasisi inayotambulika yaliyoanzishwa, yakatangazwa na kudumishwa kwa utaratibu maalum kwa ajili ya ubunifu, ujenzi, vifaa, matengenezo, ukaguzi wa meli na mifumo yake ya uhandisi na utoaji vyeti, pamoja na kutoa tafiti madhubuti kuhakikisha uhuishwaji wa vigezo vilivyotangazwa kwa lugha ya kiingereza;

"mkaguzi" maana yake ni mtu aliyeteuliwa kama mkaguzi chini ya kifungu cha 382(5) cha Sheria;

"Mkataba wa Usalama" maana yake ni Mkataba wa Kimataifa kuhusu Usalama wa Maisha Baharini wa Mwaka 1974 ikijumuisha Itifaki na marekebisho yoyote yaliyofanyika chini yake, ikiwemo Itifaki ya mwaka 1978;

"mmiliki" kuhusiana na meli, au mmiliki wa meli, maana yake ni, ikiwa ni meli iliyosajiliwa, mmiliki aliyesajiliwa na inajumuisha mkodishwaji mwenye majukumu yote na mmliki mwendeshaji au wakala mwendeshaji;

Sura ya 165 "Sheria" maana yake ni Sheria ya Usafiri Majini;

Sura ya 415 "Shirika" maana yake ni Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania lililoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania;

"taasisi zinazotambulika" maana yake ni taasisi iliyofanyiwa tathmini na shirika na kubainika kukidhi matakwa ya Kanuni ya Taasisi Inayotambulika kufanya kazi kwa naiba ya Shirika, utoaji vyeti kisheria na huduma chini ya sheria za lazima za IMO na sheria za nchi;

"tathmini" maana yake ni shughuli yoyote ya kubaini kwamba kitengo kinachotathminiwa kinakidhi masharti ya kanuni husika za kampuni iliyokasimiwa;

"ukaguzi" maana yake ni mchakato thabiti, huru na ulioandikwa wa kupata ushahidi wa ukaguzi na kutathmini malengo yake ili kubaini kiwango ambacho vigezo vya ukaguzi vinazingatiwa;

"ukaguzi na uchunguzi" maana yake ni ukaguzi na uchunguzi unaofanywa kuwa lazima kwa meli ya Tanzania au kwa mwendeshaji wa meli ya Tanzania chini ya Mikataba ya Kimataifa;

"ushahidi wa ukaguzi" maana yake ni kumbukumbu, taarifa halisi au taarifa nyingine ambayo-

(a) ni muhimu kwa vigezo vya ukaguzi na zinaweza kuthibitishwa; na

(b) inaweza kuwa na ubora au idadi;

"utoaji wa vyeti kisheria na huduma" maana yake ni utoaji wa vyeti na huduma kwa mujibu wa sheria mahususi ambazo zinajumuisha:

(a) mapitio ya michoro ya meli, ukaguzi na uhakiki

unaopelekea utoaji au, kusaidia utoaji wa cheti na au kwa niaba ya Shirika kama ushaidi wa kuzingatia vigezo vilivyomo kwenye mikataba ya kimataifa au sheria ya nchi; na

(b) vyeti vitolewavyo na taasisi inayotambulika kwa mujibu wa masharti ya kanuni ya XI-1/1 ya Mkataba wa SOLAS, na ambavyo vinaweza kujumuisha kuonyesha uzingatiaji wa masharti ya kimuundo, kimakenika na kiumeme ya taasisi inayotambulika chini ya masharti ya makubaliano yanayotambulika na Shirika;

"vigezo vya ukaguzi" maana yake ni seti ya sera, taratibu au masharti;

"wahusika wenye maslahi" maana yake ni mtu au kampuni ambayo inaweza kudhihirisha nia iliyowajibika katika mchakato wa ukaguzi na uthibitishaji, na ni pamoja na wateja wa shirika lililothibitishwa, wamiliki wa meli, waendeshaji wa meli, wajenzi wa meli, watengenezaji wa vifaa, maslahi au vyama vinavyohusiana na tasnia ya usafirishaji, maslahi au vyama vya bima ya baharini, vyama vya biashara, vyombo vya udhibiti wa kiserikali au huduma za kiserikali na mashirika yasiyo ya kiserikali;

"waraka wa MEPC" maana yake ni waraka uliotolewa na Kamati ya Kutunza Mazingira Baharini ya IMO inayoshughulikia masuala ya mazingira chini ya mamlaka ya IMO na inayojumuisha udhibiti na uzuiaji wa uchafuzi unaotoka na meli uliotajwa na mkataba wa MARPOL;

"waraka wa MSC" maana yake ni waraka uliotolewa na Kamati ya Usalama wa Baharini ya IMO ambayo inashughulikia masuala yote yanayohusiana na ulinzi na usalama baharini, ukijumuisha meli zote za abiria na aina zote za meli za mizigo; na

“Waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana na masuala ya usafiri majini.

## SEHEMU YA PILI
## MASHARTI YA UIDHINISHAJI WA TAASISI ZINAZOTAMBULIKA

Masharti ya uidhinishaji

4.-(1) Taasisi inayotambulika-

(a) haitajihusisha kwenye shughuli zozote ambazo zinaweza kukinzana na uhuru wake wa maamuzi na uadilifu na kuhusiana kwake na utoaji wa vyeti kisheria na huduma;

(b) haitakuwa mbunifu, mtengenezaji, msambazaji, mrambazaji, mnunuzi, mmiliki, mtumiaji au mtunzaji wa kitu kulingana na utoaji wa cheti kisheria na huduma, wala mwakilishi aliyeidhinishwa na mamlaka ya mmoja miongoni mwa wahusika hao;

(c) haitakuwa tegemezi kwa kiasi kikubwa kwa kampuni moja ya biashara kama chanzo cha mapato yake.

(2) Taasisi inayotambuliwa itahakikisha uzingitiwaji wa mizania ya chini ya vigezo kwa kutambuliwa kwake na Shirika kulingana na Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

Mfumo wa usimamizi wa ubora

5. Taasisi inayotambulika itaanzisha na kutekeleza mfumo wa usimamizi wa ubora na itahakikisha muendelezo wa uboreshaji na ufanisi wake kulingana na matakwa ya Kanuni hizi, masharti ya Kanuni ya Taasisi Inayotambulika na marekebisho yake yanayofuata.

Ubunifu na uendelezaji

6.-(1) Taasisi inayotambulika itapanga na kudhibiti michoro na uanzishwaji wa mchakato wa utoaji vyeti kisheria na huduma.

(2) Wakati wa kupanga na kukuza kuendeleza michoro, taasisi inayotambulika itazingazitia-

(a) hatua za kubuni na uendelezaji;

(b) mapitio, uhakiki na uthibitishaji unaofaa kwa kila huduma ya ubunifu na hatua ya uendelezaji; na

(c) majukumu na mamlaka kwa ajili ya ubunifu na uendelezaji.

(3) Taasisi inayotambulika itaruhusu ushiriki katika uendelezaji wa mapitio ya miongozo na kanuni zake hasa

katika mchakato wa mapitio kabla ya ukamilishaji, kwa wawakilishi wa Shirika na mshirika yoyote mwenye maslahi.

(4) Taasisi inayotambulika itajumuisha katika miongozo na kanuni zake masharti-

(a) yaliyoainishwa na kuwasilishwa kwa taasisi inayotambulika na shirika hususani kwa utoaji wa vyeti kisheria na huduma; na

(b) ambayo hayajatajwa na Shirika lakini ni muhimu kwa matumizi yaliyoainishwa na kukusudiwa, kama ilivyoelezwa na taasisi inayotambulika.

(5) Utekelezaji wa masharti unaweza kuwa kwa njia ya uridhiwaji kwenye masharti ya ndani ya taasisi inayotambulika kwa matumizi ya nyaraka halisi kutoka IMO au Shirika.

(6) Taasisi inayotambulika haitatoa vyeti vya kisheria kwa meli ambayo imeshushwa daraja au imebadili daraja kwa sababu za kiusalama, kabla ya kutoa fursa kwa Shirika kutoa maoni yake ndani ya muda muafaka yatakayobainisha endapo ukaguzi kamili unahitajika.

## SEHEMU YA TATU
## MAMLAKA YA KUTOA MAELEKEZO KWA TAASISI INAYOTAMBULIKA

Uteuzi na usimamizi wa taasisi inayotambulika

7.-(1) Shirika litatoa maelekezo kwa taasisi inayotambulika kufanya kazi kwa niaba yake, kuhakikisha uzingatiaji kwa meli za Tanzania na mwendeshaji wa meli ya Tanzania kwa mujibu wa vipengele husika vya nyongeza na kiambatisho cha Azimio la IMO A. 847 (20) kuhusu mwongozo wa nchi ya usajili wa meli katika utekelezaji wa mikataba na sheria za IMO.

(2) Shirika litasimamia, kuhakiki na kufuatilia kazi ya taasisi inayotambuliwa yenye mamlaka ya kufanya kazi kwa niaba yake kama ilivyoainishwa chini ya Kanuni hizi.

Majukumu ya taasisi zinazotambu lika

8.-(1) Uchunguzi, ukaguzi, uwekaji alama ya mistari ya ukomo wa ujazo, upimaji wa ujazo, ufuatiliaji wa ujenzi wa meli na kazi ya matengenezo, utoaji na uhuishaji wa vyeti husika, vyeti vya misamaha ya kudumu au ya muda

kwa utaratibu unaofanana kwa meli ya kitanzania kulingana na mikataba ya kimataifa na mkataba wa SOLAS, itatekelezwa yote kwa pamoja au kwa sehemu, na-

(a) mkaguzi wa meli; au

(b) taasisi inayotambulika iliyoidhinishwa na Shirika kufanya kazi kwa niaba yake.

(2) Katika kutekeleza majukumu ambayo yameidhinishwa na Shirika kwa mujibu wa Kanuni hizi kuhusiana na meli ya Tanzania vipengele vya mkataba wa kimataifa vinatumika, taasisi inayotambulika itahakikisha kuwa vipengele vya Kanuni hizi na Kiambatisho Na. 2 cha Kanuni ya Taasisi Inayotambulika vimezingatiwa.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), Shirika linaweza kuitaka taasisi inayotambulika kutotoa cheti chochote cha msamaha, iwe cha kudumu au cha muda, kutoka katika sharti au mipangilio inayofanana kulingana na matakwa ya mikataba ya kimataifa pamoja na utoaji na uhuishaji isipokuwa imeruhusiwa kufanya hivyo na Shirika:

Isipokuwa kwamba, Shirika litaidhinisha katika mazingira yote toleo la kwanza la vyeti vya msamaha vya awali.

(4) Bila kujali masharti yoyote ya sheria kuhusu utoaji wa vyeti, taasisi zinazotambulika hazitatoa vyeti vya kisheria kwa meli ambayo imeshushwa au kubadilishwa daraja kwa sababu za kiusalama, kabla ya kutoa fursa kwa Shirika kutoa maoni yake ndani ya muda muafaka yatakayobainisha endapo ukaguzi kamili unahitajika.

(5) Baada ya kufanya kazi ya tathmini ya usalama iliyoainishwa kuhusu mawasiliano ya radio, taasisi inayotambulika, kwa kushauriana na mamlaka husika itatoa Cheti cha Usalama wa Radio kwa Meli ya Mizigo kwa niaba ya Shirika.

(6) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (3), ili utambuzi na utekelezaji wa majukumu hayo kufanyika, taasisi inayotambulika itatekeleza vigezo vilivyoweka na shirika kwa kushauriana na mamlaka husika ambayo kwa wakati wowote vinaweza, kuondolewa pale ambapo haitekelezi tena vigezo vilivyowekwa au ufanyaji kazi wake utaonekana hauridhishi.

(7) Kanuni hii haitajumuisha utoaji vyeti wa vifaa

maalum vya baharini.

(8) Kwa madhumuni ya kanuni hii, "Cheti cha Usalama wa Radio kwa Meli ya Mizigo" maana yake ni cheti kwa jina hilo, kilichotolewa kwa kuzingatia Mkataba wa Kimataifa wa Usalama kwa mujibu wa kifungu cha 231(1)(c) cha Sheria.

Uidhinishaji wa taasisi zinazotambulika

9.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi, Shirika halitakataa kuidhinisha kufanyika kwa majukumu yoyote na taasisi zinazotambulika kama yalivyorejewa chini ya kanuni ya 8:

Isipokuwa kwamba, Shirika linaweza kuzuia idadi ya taasisi zinazotambulika ilizoziidhinisha kwa mahitaji ya usafirishaji kwa njia ya meli Tanzania, endapo kuna sababu za msingi za kufanya hivyo.

(2) Katika kutekeleleza majukumu yoyote yaliyokasimiwa kufanywa kwa niaba ya Shirika, taasisi inayotambulika-

(a) itaanzisha, itatekeleza na itadumisha ufanisi wa mfumo wa usimamizi wa ndani wa ubora ambao utakidhi masharti ya Kanuni za Taasisi Inayotambulika;

(b) litajikita kwenye maeneo stahiki ya viwango vya ubora vinavyotambulika kimataifa ambavyo ufanisi wake sio chini ya matoleo ya ISO 9000;

(c) itakidhi ubora na mfumo wa ukaguzi wa usimamizi wa mazingira; na

(d) itazingatia mahitaji ya mafunzo na ujuzi wa kiufundi kwa watumishi wa taasisi inayotambulika kulingana na kiambatisho Na. 1 cha Kanuni za Taasisi Inayotambulika.

Makubaliano na taasisi zinazotambulika

10.-(1) Shirika litaweka mahusiano ya kazi na taasisi iliyotambulika kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hizi, kwa kuingia katika makubaliano rasmi ya kimaandishi yakibainisha majukumu maalum na kazi zitakazotekelezwa na taasisi hiyo iliyotambuliwa.

(2) Mkataba ulioandikwa utasainiwa na Shirika na taasisi inayotambulika kulingana na masharti ya sheria zilizopo zinazohusu usajili na utendaji wake katika nchi ambayo taasisi inayotambulika inapatikana.

(3) Shirika litaorodhesha taasisi zinazotambulika zinazofanya kazi kwa niaba ya Shirika katika tovuti ya Shirika kwa lengo la kuujulisha umma.

(4) Mkataba uliorejewa chini ya kanuni ndogo ya (2) utakuwa kama ulivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Kanuni hizi na utajumuisha yafuatayo:

(a) vipengele vya ukaguzi wa mara kwa mara vya Shirika au vya mkaguzi binafsi aliyeteuliwa na Shirika katika majukumu yanayotekelezwa na taasisi inayotambulika yanayofanywa kwa niaba ya Shirika, kama yalivyoainishwa kwenye kanuni ya 8(1);

(b) vipengele vya uwezekano wa ukaguzi wa kawaida na wa kina wa meli;

(c) vipengele vya kuripoti kwa lazima vya taasisi inayotambulika kwa Shirika kuhusu taarifa muhimu za uwezo wa taasisi inayotambulika wa kusajili meli, mabadiliko ya daraja, kusimamishwa na kufutwa kwa cheti cha daraja;

(d) vipengele vinavyoainisha kuwa mkataba utachukuliwa kuwa umesitishwa iwapo Shirika litaiondolea utambuzi taasisi inayotambulika, kwa mujibu wa Kanuni hizi na kwa mantiki hiyo, Shirika halitawajibika kulipa fidia ya pesa kwa taasisi husika inayotambulika.

(4) Mkataba chini ya kanuni hii utakuwa na sharti kuwa taasisi inayotambulika inapaswa kuwa na mwakilishi ndani ya Tanzania Bara ambaye:

(a) amejumuishwa au kusajiliwa Tanzania Bara kulingana na sheria husika; na

(b) anaweza kufikishwa kwenye mamlaka za mahakama za Tanzania Bara.

Ufuatiliaji wa taasisi zinazotambulika

11.-(1) Katika kuhakikisha kuwa Jamhuri ya Muungano inatekeleza wajibu wake wa kimataifa kikamilifu, Shirika-

(a) litakuza, litatekeleza na kusimamia programu thabiti ya uangalizi wa taasisi inayotambulika;

(b) litafuatilia kazi ya taasisi inayotambulika kwa:

(i) kufanya ukaguzi wa ziada ili kuhakikisha kuwa meli inayopaswa kupeperusha bendera

ya Jamhuri ya Muungano inakidhi-

(aa) masharti ya mikataba ya kimataifa inayotumika;

(bb) masharti ya kitaifa, yanayohusiana na masharti ya lazima ya kimataifa; na

(ii) kuwa na wafanyakazi ambao-

(aa) wana uelewa wa sheria na kanuni za Jamhuri ya Muungano na wa Taasisi Inayotambulika; na

(bb) wapo tayari kufanya usimamizi thabiti wa uangalizi wa taasisi inayotambulika.

(2) Shirika litasimamia majukumu yaliyokasimiwa kwa taasisi inayotambulika kwa kuzingatia yafuatayo:

(a) utunzaji wa nyaraka za mfumo wa usimamizi wa ubora;

(b) upatikanaji wa maelekezo ya ndani, waraka na miongozo ya taasisi inayotambulika;

(c) upatikanaji wa nyaraka za taasisi inayotambulika zinazohusiana na meli za Jamhuri ya Muungano;

(d) ushirikiano kwa kaguzi za Shirika na uthibitisho wa kazi; na

(e) utoaji wa taarifa na takwimu kama vile, uharibifu na majeruhi wanaohusiana na meli ya Jamhuri ya Muungano.

(3) Shirika litaweka mfumo wa kuhakikisha kuwa utoaji wa vyeti kisheria na huduma unaotolewa unajitosheleza na unazingatia Kanuni za Taasisi Zinazotambulika.

(4) Shirika litapaswa-

(a) kufanya ufuatiliaji angalau mara moja kwa mwaka; na

(b) kuandaa ripoti ya matokeo ya ufuatiliaji katika mwaka unaofuata mwaka ambao ufuatiliaji ulifanyika.

Wajibu wa Shirika katika kufanya ukaguzi wa meli za nje TS. Na. 67 ya 2019

12.-(1) Endapo wakati wa kutekeleza haki na wajibu wa ukaguzi chini ya Kanuni za Ukaguzi wa Meli za Nje za Uwakala wa Meli Tanzania, itathibitika kuwa-

(a) taasisi inayotambulika, inayofanya kazi kwa niaba ya nchi ya usajili wa meli, imetoa cheti halali kwa meli ambayo haikidhi masharti husika ya Mikataba ya Kimataifa; au

(b) meli yenye cheti cha daraja halali ina upungufu au kushindwa kuendana na vipengele vilivyoainishwa katika cheti husika,

Shirika litatoa taarifa ya makosa hayo kwa-

(i) nchi ya usajili wa meli husika; na

(ii) taasisi husika inayotambulika wakati wa ukaguzi wa awali.

(2) Taarifa inayotolewa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1)-

(a) itahusu kugundulika kwa meli yenye viashiria hatarishi kwa usalama na mazingira; au

(b) itaonesha ushahidi wa tabia ya uzembe wa taasisi husika inayotambulika.

(3) Nchi husika ya usajili na taasisi inayotambulika zilizojulishwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) itakuwa na wajibu wa kuchukua hatua za ufuatiliaji mara moja.

Wajibu wa mmiliki wa meli

13.-(1) Mmiliki wa meli ya Tanzania:

(a) atahakikisha kuwa meli imebuniwa, imejengwa, imewekewa na kutunzwa kwa kuzingatia kanuni na miongozo ya taasisi inayotambulika kuhusiana na umbo la meli, ufungaji wa mitambo na mifumo ya vifaa vya umeme na udhibiti vya taasisi inayotambulika iliyoidhinishwa; na

(b) ataweka kwenye meli cheti cha daraja halali kinachotolewa na taasisi inayotambulika.

(2) Shirika litapaswa-

(a) kushirikiana na taasisi inayotambulika katika kuandaa kanuni na taratibu za taasisi hiyo; na

(b) kukubaliana na taasisi inayotambulika ili kufikia tafsiri sawa ya Mikataba ya Kimataifa.

(3) Mmiliki na mwendeshaji wa meli ya Tanzania ambaye atakaidi au atashindwa kuzingatia masharti ya meli kama yalivyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1) atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi dola za Marekani elfu tano au kiwango kinacholingana katika shilingi za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Wajibu wa Msajili

14.-(1) Msajili-

(a) atahifadhi nakala za Mikataba ya Kimataifa iliyorejewa katika kanuni ndogo ya (2); na

(b) atatoa kwa mtu yeyote anayehitaji-

(i) kupata Mkataba wowote wa Kimataifa, ikiwa mtu huyo anayehitaji atazingatia utaratibu ulioainishwa katika taarifa; na

(ii) nakala ya Mikataba hiyo ya Kimataifa, ikiwa mtu huyo anayehitaji atazingatia utaratibu ulioainishwa katika taarifa na kulipa kwa Msajili ada iliyoainishwa na Msajili, isiozidi gharama iliyotumika na Shirika katika maandalizi ya nakala hiyo.

(2) Mikataba ya Kimataifa ambayo Msajili ana jukumu nayo chini ya kanuni ndogo ya (1) ni pamoja na-

(a) Mikataba ya Kimataifa, katika matoleo yao ya sasa, ikiwa inaruhusiwa na haki miliki za IMO, Shirika la Kazi la Duniani na Umoja wa Kimataifa wa Mawasiliano;

(b) Maazimio na waraka wa IMO, zilizorejewa katika Kanuni hizi.

(3) Msajili anaweza kuhifadhi nakala ya Mikataba ya Kimataifa, iliyorejewa chini ya kanuni ndogo ya (2) kwa mfumo wa kielektroniki au karatasi.

Kukataa, kufutwa au kusimamishwa kwa uidhinishaji wa taasisi inayotambulika

15.-(1) Bila kuathiri vigezo vya chini vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi, pale ambapo Shirika litaona kuwa taasisi inayotambulika haipaswi tena kuidhinishwa kufanya kazi kwa niaba yake, linaweza kusimamisha au kufuta uidhinishaji huo.

(2) Shirika litaitaarifu taasisi inayotambulika kuhusiana na nia yake ya kusimamisha au kufuta na kuijulisha kuhusu sababu zinazopelekea kufanya hivyo na kuipa taasisi hiyo haki ya kuwasilisha wawakilishi ndani ya siku saba za kazi kuanzia tarehe ya taarifa hiyo.

(3) Shirika, katika kutoa uamuzi wake, litaitaarifu IMO kuhusu uamuzi husika chini ya kanuni ndogo ya (1) bila kuchelewa na kwa kutoa sababu za msingi za uamuzi huo.

(4) Kusimamisha au kufuta uidhinishaji kutatekelezwa kupitia uamuzi wa Shirika kwa kuchapishwa

kwenye tovuti ya Shirika.

(5) Pale ambapo Shirika litasimamisha au kufuta idhini, litaitaarifu taasisi husika inayotambulika kuhusu uamuzi wake.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA JUMLA

Adhabu ya jumla

16. Mtu yeyote anayekiuka masharti yoyote ya Kanuni hizi ambayo hakuna adhabu maalum iliyoainishwa, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua dola za Marekani elfu mbili na isiyozidi dola za Marekani elfu kumi au kiwango sawa katika shilingi za Kitanzania.

Kipindi cha mpito

17. Cheti au nyaraka iliyotolewa kwa meli ya Tanzania au mmiliki wa meli kabla ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi itaendelea kuwa halali hadi tarehe ya ukomo wa cheti hicho au nyaraka husika.

Mipaka ya majukumu ya taasisi inayotambulika

18. Shirika halitaruhusu au kukasimisha kwa taasisi inayotambulika-

(a) majukumu yaliyo juu ya uwezo wake kwa kuzingatia vipengele vya Kiambatisho Na. 2 cha Kanuni za Taasisi Inayotambulika, kutoa idhini; na

(b) kuhudumia meli, isipokuwa zilizosajiliwa chini ya Sheria, masharti yoyote kuhusiana na Kanuni za daraja lake, masharti, kanuni au viwango vya utendaji wa daraja zilizopo, zaidi ya matakwa ya Mikataba ya Kimataifa.

Ushirikiano kati ya taasisi zinazotambulika

19.-(1) Pale ambapo utoaji wa cheti kisheria kwa meli utahamishwa kutoka taasisi inayotambulika kwenda taasisi nyingine, taasisi inayohamisha, bila kuchelewa, itatoa ruhusa kwa taasisi inayohamishiwa historia ya mafaili ya meli pamoja na-

(a) uchunguzi ambao haujafanyika;

(b) mapendekezo ya uchunguzi wowote ambao haujafanyika na hali ya daraja la meli;

(c) masharti ya uendeshaji yaliyotolewa kwa meli;

(d) mipaka ya uendeshaji iliyotolewa dhidi ya meli; na

(e) taarifa za kiufundi, michoro, mipango na nyaraka kwa kuzingatia miongozo iliyoandaliwa na taasisi inayotambulika.

(2) Vyeti vipya vya meli vinaweza kutolewa na taasisi inayopokea inayotambulika baada ya kukamilika kikamilifu kwa uchunguzi na mapendekezo ya daraja uliotolewa awali kuhusiana na meli umekamilika kama ulivyobainishwa na taasisi iliyotoa inayotambulika.

(3) Ndani ya mwezi mmoja baada ya kutolewa kwa vyeti, taasisi inayopokea inayotambulika itaishauri taasisi iliyotoa inayotambulika kuhusu tarehe ya utoaji vyeti na kudhibitisha tarehe, mahali na hatua zilizochukuliwa kujiridhisha kuhusu uchunguzi ambao haukufanyika, mapendekezo ya uchunguzi ambayo hayakufanyika na hali ya daraja la meli.

(4) Taasisi inayotambulika itaweka na kutekeleza masharti stahiki ya pamoja kuhusu masuala ya uhamishaji wa utoaji wa vyeti kisheria ambapo tahadhari maalum ni muhimu, ikijumuisha-

(a) utoaji vyeti kisheria kwa meli zenye miaka 15 au zaidi; na

(b) uhamishaji wa meli kutoka kwa taasisi inayotambulika isiyotambulika na Shirika.

Tathmini na utoaji wa taarifa

20.-(1) Msajili-

(a) atafanya tathmini ya masharti ya udhibiti yaliyomo katika Kanuni hizi;

(b) atandaa taarifa inayoainisha hitimisho la tathmini; na

(c) atawasilisha taarifa hiyo kwa Waziri.

(2) Taarifa ya kwanza chini ya kanuni hii itachapishwa kabla ya mwaka wa tano wa maadhimisho ya siku ambayo Kanuni hizi zitaanza kutumika.

(3) Taarifa zinazofuata zitachapishwa kwa kipindi kisichozidi miaka mitano.

(4) Taarifa iliyoandaliwa na kuwasilishwa chini ya kanuni hii-

(a) itaainisha malengo yanayokusudiwa kufikiwa na masharti ya udhibiti yaliyoainishwa chini ya

kanuni ndogo ya (1)(a);

(b) itatathmini kiwango ambacho malengo hayo yanafikiwa;

(c) itatathmini endapo malengo yaliyoainishwa yana tija; na

(d) pale ambapo malengo yanatija, taarifa itatathmini kiwango ambacho yanaweza kufikiwa kwa njia nyingine inayohusisha masharti mepesi ya udhibiti.

Ushughulikiaji wa malalamiko TS. Na. 338 ya 2018

21. Mtu ambaye hajaridhika na uamuzi uliotolewa chini ya Kanuni hizi anaweza kutuma maombi ya mapitio kwa Shirika kwa mapitio kwa mujibu wa Kanuni za Ushughulikiaji wa Malalamiko za Wakala wa Meli Tanzania.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni za 4(2) na 15(1))*

VIWANGO VYA CHINI VYA UTAMBUZI WA TAASISI ZINAZOTAMBUKA

A. Viwango vya Chini vya Jumla

1. Taasisi inayotambulika inapaswa kuwa imesajiliwa kisheria katika nchi iliyopo. Hesabu zake zitathibitishwa na wakaguzi huru.

2. Taasisi inayotambulika itakuwa na uwezo wa kuhifadhi taarifa za uzoefu wa kina katika kutathmini ubunifu na ujenzi wa meli.

3. Taasisi inayotambulika inapaswa kuwa na uwezo wakati wowote wa wafanyakazi katika kada ya uongozi, utaalam, usaidizi, utafiti unaolingana na ukubwa wa daraja, muundo wake na ushiriki wa shirika katika ujenzi na ubadilishaji wa meli.

4. Taasisi inayotambulika itakuwa na uwezo wa kupanga katika kila eneo la kazi, kwa wakati na kama inavyohitajika, nyenzo na wafanyakazi kulingana na kazi zitakazofanyika kwa mujibu wa vigezo vya jumla vya chini ya alama 6 na 7 na kwa vigezo maalum vya chini ya sehemu hii.

5. Taasisi inayotambulika itakuwa na itatumia seti za sheria na taratibu zake binafsi, au uwezo wake uliooneshwa, wa ubunifu, ujenzi na ukaguzi wa kipindi maalum wa meli, wenye kuzingatia ubora wa viwango vinavyotambulika kimataifa. Zitachapishwa na kuendelea kuboreshwa na kuongezewa viwango kwa kupitia tafiti na programu za maendeleo.

6. Taasisi inayotambulika itakuwa na rejesta ya meli itakayochapishwa kila mwaka au kutunzwa katika kanzi data ya kielektroniki itakayopatikana kwa umma

7. Taasisi inayotambulika haitaendeshwa na wamiliki wa meli au wajenzi wa meli, au yeyote anayejihusisha kibiashara katika uzalishaji, uwekaji vifaa, ukarabati au uendeshaji wa meli. Taasisi inayotambulika haitegemei kampuni moja ya kibiashara kama chanzo kimoja cha mapato yake. Taasisi inayotambulika haitafanya kazi katika daraja au kazi ya kisheria ikiwa inafanana na au ina biashara binafsi au yenye muunganiko wa kifamilia na mmiliki wa meli au mwendeshaji. Masharti haya pia yatatumika kwa wakaguzi walioajiriwa na Taasisi inayotambulika.

8. Taasisi inayotambulika itafanya kazi kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa katika Kiambatisho cha Azimio la IMO A.789(19) cha vigezo vya ukaguzi na uthibitisho wa majukumu ya Taasisi inayotambulika inayofanya kazi kwa niaba ya nchi ya usajili, kwa kuwa inatekeleza masuala yaliyo chini ya Kanuni hii.

B. Vigezo Maalum vya Chini

1. Taasisi inayotambulika itakuwa na mtandao wake duniani kote kwa kupitia wakaguzi wake, au vinginevyo, katika mazingira yanayokubalika, kupitia wakaguzi wa Taasisi nyingine inayotambulika.

2. Taasisi inayotambulika itaongozwa na kanuni za maadili kwa mujibu wa Kanuni ya Taasisi Inayotambulika.

3. Taasisi inayotambulika itaendeshwa na kusimamiwa kwa namna ambayo itahakikisha usiri wa taarifa kama inavyotakiwa na nchi ya usajili.

4. Taasisi inayotambulika itatoa taarifa husika kwa Shirika na kwa wahusika wenye maslahi.

5. Taasisi inayotambulika, wakaguzi wake na wafanyakazi wake watafanya kazi zao bila kuathiri kwa namna yoyote haki miliki za chelezo, wasambazaji wa vifaa na wamiliki wa meli, ikijumuisha hati miliki, leseni, ujuzi, au aina yoyote ya ujuzi ambao matumizi yake yanalindwa kisheria katika ngazi ya kimataifa au kitaifa. Katika hali yoyote, na bila kuathiri mamlaka ya tathmini ya Jamhuri ya Muungano, taasisi inayotambulika au wakaguzi na wafanyakazi, ambao imewaajiri hawapaswi kusambaza au kufichua taarifa husika kibiashara zilizopatikana wakati wa ukaguzi, kuangalia na kutathmini meli zinazojengwa au kukarabatiwa.

6. Menejimenti ya taasisi inayotambulika itafafanua na kuifadhi sera na malengo yake, kudhamiria katika ubora na itahakikisha kuwa sera hiyo inaeleweka, kutekelezwa na kudumishwa katika ngazi zote za taasisi inayotambulika. Sera ya taasisi inayotambulika itarejea malengo na viashiria vya utendaji wa usalama na uchafuzi wa mazingira.

7. Taasisi inayotambulika itahakikisha-

(a) sheria na kanuni zake zimewekwa na kutunzwa kwa utaratibu maalum;
(b) kanuni na miongozo yake inazingatiwa na mfumo wa ndani wa kupima ubora wa huduma kuhusiana na kanuni na miongozo hiyo umewekwa;
(c) masharti ya kazi ya kisheria ambayo taasisi inayotambulika imekasimiwa yanaridhisha na mfumo wa ndani wa kupima ubora wa huduma kuhusiana na uzingatiaji wa mikataba ya kimataifa umewekwa;
(d) majukumu, mamlaka na mwingiliano wa watumishi ambao kazi zao zinaathiri ubora wa huduma katika taasisi inayotambulika yanafafanuliwa na kuhifadhiwa;
(e) kazi zote zinafanyika chini ya masharti yaliyowekwa;
(f) mfumo wa usimamizi umewekwa ambao unafuatilia vitendo na kazi zinazofanywa na wakaguzi na watumishi wa kitaalam na utawala walioajiriwa na taasisi inayotambulika;
(g) wakaguzi wana ujuzi wa kutosha katika aina fulani ya meli ambayo wanafanya kazi zao husika kwa ukaguzi fulani utakaofanyika na kwa kufuata masharti husika;
(h) kumbukumbu zinatunzwa, kuonesha mafanikio ya viwango vinavyotakiwa katika maeneo yalifanyiwa huduma, pamoja na ufanisi wa uendeshaji wa mfumo wa ubora;
(i) mfumo unaojitosheleza wa mpango na utunzaji wa kaguzi za ndani kwa shughuli zinazohusiana na ubora unakuwa katika maeneo yote;
(j) kaguzi za kisheria zinazohitajika na mfumo wa pamoja wa ukaguzi na utoaji vyeti ambavyo taasisi inayotambulika imeidhinishwa zinafanyika kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa katika Kiambatisho cha Azimio la IMO A.948 (23); na
(k) mipaka ya wazi ya uwajibikaji na udhibiti inawekwa kati ya ofisi kuu na ofisi za kanda za taasisi inayotambulikana na kati ya taasisi zinazotambulika na wakaguzi wao.

8. Taasisi inayotambulika itakuwa na mfumo wa ubora ulioendelezwa, unaotekelezeka, kwa kuzingatia maeneo sahihi ya mfumo wa ubora wa ndani unaotambulika kimataifa na kwa kuzingatia Kanuni za Taasisi Zinazotambulika katika mifumo ya usimamizi wa ubora, masharti kama yalivyotafsiriwa na kuthibitishwa na chombo kinachoidhinisha tathmini ya ubora.

9. Kanuni na miongozo ya taasisi inayotambulika itatekelezwa kwa namna ambayo taasisi inayotambulika itabaki kuwa katika nafasi ya kujielekeza katika maudhui ya ujuzi wake na uamuzi wa kuaminika na tamko lenye mantiki katika usalama wa meli husika kwa njia ya cheti cha daraja katika misingi ambayo cheti cha kisheria kinaweza kutolewa.

10. Kwa kuwatumia watumishi wenye sifa za kitaalum na kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa katika Kiambatisho cha Azimio la IMO A.913(22), taasisi inayotambulika itakuwa na njia madhubuti ya kutathmini matumizi na matengenezo ya mfumo wa usimamizi wa usalama, popote nchi kavu na melini, palipokusudiwa kuhusishwa katika utoaji cheti, zilizokusudiwa kuhusishwa katika utoaji cheti.

11. Taasisi inayotambulika itaruhusu ushiriki katika uandaaji wa sheria na kanuni zake na wawakilishi wa utawala na vyama vingine husika.

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 10(4))*

VIPENGELE VYA KUJUMUISHWA KATIKA MAKUBALIANO KATI YA SHIRIKA NA TAASISI ZINAZOTAMBULIKA

Vimeandaliwa kwa mujibu wa Kiambatisho 2 cha Azimio la IMO A.739 (18) na Kiambatisho 3 cha Kanuni ya RO, Annex, Viambatisho na Kiambatisho kwa IMO MSC / Mviringo 710 na MEPC / Nyaraka 307

Makubaliano rasmi ya kimaandishi kati ya Shirika na taasisi inayotambulika yatajumuisha yafuatayo:

1. Maombi.

2. Madhumuni.

3. Masharti ya jumla.

4. Utekelezaji wa kazi chini ya idhini:
(a) kazi kwa mujibu wa idhini ya jumla;
(b) kazi kwa mujibu wa idhini maalum (ya ziada);
(c) uhusiano kati ya sheria ya taasisi inayotambulika na shughuli nyingine zinazohusiana; na
(d) kazi za kushirikiana na Nchi za Bandari ili kuwezesha urekebishaji wa upungufu wa udhibiti wa Serikali ya Bandari ulioripotiwa au tofauti ndani ya ufuatiliaji wa taasisi inayotambulika.

5. Msingi wa kisheria wa kazi chini ya idhini:
(a) Sheria, kanuni na masharti ya nyongeza;
(b) tafsiri; na
(c) ukiukaji na ufumbuzi wa ukiukaji.

6. Taarifa kwa nchi ya bendera:
(a) taratibu za kutoa taarifa katika idhini ya jumla;
(b) taratibu za kutoa taarifa katika kibali maalum;
(c) kutoa taarifa juu ya uainishaji wa meli (mgao wa daraja, mabadiliko na ufutaji), kama inavyotumika; na
(d) kutoa taarifa ya matukio endapo meli ina hitilafu inayosababisha meli kushindwa kuendelea na safari bila kusababisha hatari kwa meli au watu waliokuwemo au kubainika kuwa na viashiria vya uharibifu wa mazingira; na
(e) taarifa nyingine.

7. Uandaaji wa sheria na kanuni – taarifa:
(a) ushirikiano kuhusiana na uandaaji wa sheria na kanuni – mikutano ya mahusiano;
(b) kubadilishana sheria na kanuni na taarifa; na

(c) lugha na muundo.

8. Masharti mengine:
(a) malipo;
(b) kanuni za masharti ya kiutawala;
(c) usiri;
(d) madai ambayo yatajumuisha taasisi inayotambulika na wafanyakazi wake wanaohusika au kuwajibika katika utoaji wa uidhinishaji wa kisheria na huduma inaweza kutakiwa na sheria husika kugharamiwa na fidia ya kitaaluma au bima ya dhima ya kitaaluma katika tukio ambalo dhima hiyo itatolewa kwa Jamhuri ya Muungano kwa hasara au hasara ambayo imethibitishwa katika mahakama kuwa imesababishwa na kitendo chochote cha uzembe au kutotenda kazi kwa taasisi yake inayotambulika. Kuhusiana na hili, Shirika linaweza pia kuzingatia kuweka kizuizi kwa kiwango cha dhima na ulipaji kitakacholipwa chini ya bima hiyo au mipango mingine ya fidia;
(e) wajibu wa kifedha;
(f) kuanza kutumika;
(g) usitishaji;
(h) uvunjaji wa makubaliano;
(i) utatuzi wa migogoro;
(j) kutumia kandarasi ndogo;
(k) kupatiwa makubaliano; na
(l) marekebisho.

9. Ufafanuzi wa idhini kutoka Shirika kwenda kwa taasisi inayotambulika:
(a) aina na ukubwa wa meli;
(b) mikataba na nyaraka nyingine, ikiwa ni pamoja na sheria husika za kitaifa;
(c) kuidhinishwa kwa michoro;
(d) kuidhinishwa kwa vifaa;
(e) ukaguzi;
(f) utoaji wa vyeti;
(g) marekebisho;
(h) usitishwaji wa vyeti; na
(i) kuripoti.

10. Usimamizi wa majukumu ya taasisi inayotambulika unaofanywa na Shirika:
(a) nyaraka za mfumo wa uhakiki wa ubora;
(b) upatikanaji wa maelekezo ya ndani na miongozo;
(c) upatikanaji wa nyaraka za taasisi inayotambulika zinazohusiana na meli ya Jamhuri ya Muungano kwa Shirika;
(d) kushirikiana katika kazi ya ukaguzi na uhakiki na Shirika; na
(e) utoaji wa taarifa na takwimu, mathalani, kuhusu uharibifu na majeruhi wanaohusika na meli ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Dodoma,
28 Juni, 2023

MAKAME M. MBARAWA,
*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi*